# NI MWEZI WA ROZARI

Jovin A. Banturaki
Wichita City, Sept.2018

♩ = 75






1. Ni wakati mzuri kumtukuza Maria
   Mama wa Mungu, na kumuomba mazuri yake,
   Bikira, Bikira mwenye huruma
   Mama utuzawadie mazuri
   Mama utuzawadie tuombayo.

2. Ni wewe Mama yetu, tunakukimbilia
   Utupokee, utufikishe kwa Bwana Yesu
   Mwanao Mwokozi wetu kwa damu
   Mama, utujaze furaha zako
   Mama, tufaidike na mapenzi yako.

3. Amani, utulivu, utujalie Mama
   N-chini mwetu, utuepushe maovu yetu
   Dumisha upendo, haki na usawa
   Mama, na umoja wetu udumu
   Mama, Tanzania mikononi mwako.

4. Ee mama uzilinde, familia za kwetu
   kwa mapenziyo, zijazwe na mwanga wa Mwanao
   Rozari, ibada ya familia
   Mama, ukuze ibada ya kweli
   Mama, ubariki familia zetu.

5. Kanisa letu Mama, lihimili dhoruba
   Lisidhurike, chini ya ulinzi wako Mama
   Lidumu imara ulimwenguni,
   Mama na litufundishe ya kweli
   Mama, Kanisa ni tegemeo letu.

6. Tumtukuze Maria, kwa kusali Rozari
   Ibada nzuri, tutoe masifu yetu kwake
   Malkia wa mbingu na ufurahi
   Mama, twapenda sana kukuona
   Mama, maisha yetu uyabariki.